**KISWAHILI**

**KIDATO CHA TATU**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**MTIHANI WA KATI YA MUHULA 2 2025**

**UFAHAMU (Ala.10)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Mengi yamesemwa kuhusiana na chi kuwa na katiba mpya. Kile ambacho hakibainiki hasa, ni jinsi ambavyo wanasiasa wetu wamejitwalia nafasi ya ukunga na tena ya uzazi na mama mwenye mtoto kutupwa pembeni. Je, huyu si mtoto wa Wanjiku tena?

Huenda visa vya hivi karibuni vinavyohusu familia mbalimbali vikawa na mizizi katika huyu mwana wa Wanjiku. Si haba unasikia kisa cha baba ambaye amemwua mwanawe na kumkatakata mapandemapande na kuyaacha yaoze yakiozeana kwa sababu ya msinyo au msakamo. Akili za binadamu zinapolazimishwa kwenda Zaidi ya uwezo wa kawaida, matokeo aidha ni kuingiwa na wazimu, yaani kupagawa, au kuua bila kukusudia.

Aidha, kuna wengi wengine ambao huyachukua maisha yao wenyewe kwa kutaka kuondokewa na shida. Hawa husabau kuwa mbio za sakafuni huishia ukingoni. Si nadra kwa hivyo kuwa na viumbe wanaojitia kitanzi mara kwa mara ili kuepuka mg'ang'ano wa maisha yasiyo na matumaini katu. Je, hali hii itaendelea hadi lini?

Muujiza mwingine ni ule wa ubakaji wa watoto na maajuza. Nyanya tena si mpezi aliyekusanyiwa watoto na vijana wa kata nzima jioni na wakazunguka mtoto wake na kushiba ngano zake ambazo zilikuwa hazina mwisho. Si nyanya mabaye zao lake kuu lilikuwa viazi vitamu na njugu karanga kwa minajili ya kuwalisha wajukuu wake jioni, na asubuhi, kama ndege kuonja umande wa asubuhi? Leo nyanya anaishi na uwoga, hawaamini tena wajukuu ni wabakaji. Sasa vipi chamichemi ya furaha kugeuzwa simanzi ya huzuni? Wasemao husema, dunia uwanja wa fujo.

Ukizuru magereza yetu ndipo tuna shida katika nchi yetu. Watu wamefungiwa tumbitumbi. Hadithi zao nazo ni nyingi; uvutaji bagi, wizi wa kimabavu, kuua jamaa, uchopozi na Zaidi. Hakuna mwisho.

Ashakum si matusi, ugonjwa wa "kidon" umeanza kuwashika ndugu zetu vilivyo. Asilimia ya watu wanashikwa wakilangua dawa za kulevya haisemeki. Wote huwa na jibu lilelile. Maisha yamekuwa ghali na hapana ila kutumia kila mbinu. Je, hatujaambiwa uhalifu haulipi chochote?

Kukariri usemi huo wa Leonard Mambo Mbotela na wengine wenye semi kama hizo wakiwemo wahubiri mbalimbali ni Baraka maana hupunguza makali ya maisha na kutoa nafasi ya kutabasamu kidogo, ijapo siku moja.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

CamScanner

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

***Maswali***

1. Taja na ueleze kisa chochote kinachoonyesha msinyo kulingana na mwandishi (Ala.1)

- Mzazi kumuua mwanawe - Ubakaji
- Kuwa wazimu
- Kuua bila kukusudia au kujinyonga (1x1=1)

2. Kwa nini mwandishi anawalaumu wanasiasa? (Ala.2)

Wao ndio wamewanyima watu katiba na kuwasababishia wengi msinyo.

3. Kulingana na taarifa hii nyanya alikuwa na wajibu gani? (Ala.2)

- mlezi wa watoto
- Aliwaburudisha kwa ngano
- Aliwalisha wajukuu wake
- Alipanda viazi na njugu alizowapa kila siku. (1x2 =2)

4. Wajibu wa nyanya umegeuzwa na watoto na vijana wenyewe kivipi? (Ala.2)

Wamekuwa wabakaji na kumfanya nyanya kuishi kwa woga. (1x1=1)

5. Safari ya jela imedhihirisha uvumbuzi gani muhimu? (Ala.2)

- Waliofungiwa huko ni watu wengi sana, wenye misingi ~~tofauti tofauti~~
- Wengi walishikiwa wakilangua dawa za kulevya. (1x2=2)

6. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa (Ala.2)
   a) Msakamo

   udhia

   b) Uchopozi

   wizi

(2x1=2)

**MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

a) Taja mifano miwili ya viyeyusho (Ala.2)

/w/ na /y/

b) Sauti hizi zina usawa gani? (Ala.2)

i) /b/ na /t/ — ni vipasuo/vizuio/vizuiwa

ii) /m/ na /ng'/ — ni nazali/vipuo/ving'ong'o

c) i) Nini maana ya silabi? (Ala.1)

pigo moja la sauti katika neno

ii) Tenganisha silabi katika neon lifuatalo (Ala.2)
mlolongo

m – lo – lo – ngo

d) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi (Ala.2)

i) Rithi — Urithi / mridhi / uradhi



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

CamScanner

ii) Soma

Somo/Msomaji/Usomaji

e) Ainisha viwakilishi katika sentensi ifuatayo (Ala.2)

Mwenyewe amekubali yote

mwenyewe – cha pekee kuonyesha kusisitiza

yote – cha pekee kuonyesha bila kubakisha/jumla

f) Eleza matumizi ya na katika sentensi hizi (Ala.2)

i) Lovine na Levina ni watoto wazuri

Kiunganishi

ii) Vijana watukutu waliadhibiwa na mwalimu

Kihusishi cha mtenda

g) Tunga sentensi ukitumia neno kitoto kama: (Ala.2)

i) Nomino

Kitoto hiki hakiwezi kujilisha.

ii) Kielezi

Juma ni mkubwa lakini hufanya mambo yake kitoto.

h) Andika sentensi hii katika usemi taarifa (Ala.2)

"Njoo hapa mara moja!" Ali aliamriwa na baba yake.

Baba yake alimwamuru aende hapo mara moja/bila kusita.

i) Kanusha sentensi ifuatayo katika umoja. (Ala.2)

Sisi ndio tunaopenda kula ndizi.

Sisi sio tunaopenda kula ndizi.

Sisi ndio tusiopenda kula ndizi.

j) Tofautisha sentensi hizi: (Ala.2)

i) Kitabu chote kitasomwa

Kitabu kwa jumla/bila kubakisha

ii) Kitabu chochote kitasomwa

Kitabu bila kubagua/bila kuchagua

k) Andika katika udogo (Ala.2)

Ng'ombe aliyeanguka mtoni alivunjika mguu

Kigombe kilichoanguka kijitoni kilivunjika kiguu.

l) Nomino hizi ziko katika ngeli gani? (Ala.3)

i) Nyua – U–ZI

ii) Kiwete – A –WA



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

CamScanner

iii) ugonjwa — U-YA

m) Sahihisha sentensi hizi: (Ala.2)

i) watu wagani walichukua ng'ombe zetu

Watu gani walichukua ng'ombe wetu?
Watu wapi/wepi walichukua ng'ombe wetu?

ii) walipika machakula nyingi siku ya harusi

Walipika chakula kingi siku ya harusi.
Walipika vyakula vingi siku ya harusi.

n) Kanusha sentensi hizi (Ala.2)

i) Mkungu uliokatwa umebebwa

~~Mkungu uliongwa umetubwa.~~
Mkungu ambao haukukatwa haukubebwa.

ii) Nikipata nauli nitasafiri

~~Nikikosa nauli~~
Nisipopata nauli sitasafiri.

**A. ISIMU JAMII (Ala.5)**

Eleza sifa tano za lugha

(i) Kila lugha ina sauti zake.
(ii) Kila lugha ina wazungumzaji wake
(iii) Lugha hubadilika kulingana na mazingira na wakati.
(iv) Hakuna lugha bora kuliko nyingine.
(v) Lugha huzaliwa na inaweza kufa
(vi) Lugha hukua

**B. FASIHI SIMULIZI (Ala.5)**

Orodhesha vipera vitano vya utanzu wa semi

(i) Methali
(ii) Vitendawili
(iii) Chemshabongo
(iv) Mafumbo
(v) Vitanza ndimi
(vi) Lakabu
(vii) Shirikina
(viii) Misimu
(ix) Nahau
(x) Misemo



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

CamScanner